


# HALMASHAURI YA WILAYA LONGIDO.

Barua zote ziandikwe kwa  
Mkurugenzi Mtendaji  
Halmashauri ya wilaya Longido  
Simu No. 027 - 2539603/2.



S.L.P 84  
LONGIDO,  
MKOA WA ARUSHA.

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI KWA KADA YA UDEREVA

### DARAJA LA II NAFASI 2.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido anawatangazia Watanzania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido kuomba kazi ya Udereva daraja la II. Kama inavyoonekana hapa chini:-

#### 1.0 DEREVA DARAJA LA II.

##### 1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji anatakiwa awe na sifa zifuatazo:-

1. Awe amehitimu kidato cha nne (IV) na kufaulu
2. Awe na leseni daraja la C au E ya uendeshaji wa magari ambayo ameifanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja
3. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na NIT, VETA au chuo chochote kinachotambuliwa na serikali
4. Mwombaji awe na cheti cha majaribio ya ufundi daraja la II (Trade Test grade II)

##### 1.1.2 MAJUKUMU YA KAZI

- Kukagua gari kabla na baada ya kuanza safari ili kubaini hali ya usalama wa gari,
- Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi,
- Kujaza na kutunza taarifa zote katika daftari la safari (log book)
- Kufanya usafi wa gari,
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,

➤ Kutambua na kuthibitisha ubovu katika mashine na kutoa taarifa.

### **1.1.3 MSHAHARA**

Ngazi ya mshahara ni TGS B -1 yaani Tshs 390,000.00

### **MASHARTI YA JUMLA.**

- i. Mwombaji awe na umri usiozidi miaka 45
- ii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayo jitosheleza (Detailed C.V)
- iii. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu, cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (Passport Size) na kila picha iandikwe jina nyuma.
- iv. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU na NECTA).
- v. Uwasilishaji wa taarifa za kugushi wahasika watachukuliwa hatua za kisheria.
- vi. Waombaji wote wanalazimika kuwa na namba ya utambulisho wa Uraia (National Identification Number) kutoka mamlaka ya vitambulisho ya Taifa (NIDA)

**Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 10 Mei, 2022 saa 9.30**

Maombi yanaweza kuandikwa kwa Lugha ya Kiswahili au Kiingereza na kuwasilishwa Masjala bayana ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido au kwa njia ya posta kwa kutumia anwani ifuatayo.

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
S.L.P. 84,  
LONGIDO.**



**MBOYA E.W  
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA  
LONGIDO.**

